# Masomo Ya Biblia
# kwa
# KANISA LA ELOHIM (COG)
# Siku Ya Saba (7th day)

---

## Robo Ya Kwanza
## 2026

---

## Ya
## Januari, Februari, Machi.
## (Tevet, Shevat, Adar, Abib)
## Ya
## Kutumiwa na Biblia

---

**Watenda kazi wanahitajika, Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache...**

---

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568,**
**Jerusalem - Israel**

------------------------------------------------------------

### Somo la Januari 3, 2026 (Tevet 14, 5786).
### AHADI KWA WASHINDI PEKEE

**Somo Kuu: Ufunuo 2:1-17**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 2:11.**

1. Je! Neno "mshindi" linamaanisha nini? Mwanzo 32:24-28
2. Jinsi gani Paulo alituambia tushinde? Warumi 12:21.
3. Je! Ni nini tunapaswa kufanya ili tupate ushindi juu ya dhambi na majaribu? 1 Yohana 5:4,5.
4. Je! Malaika alimwambia nini Yakobo baada ya kupambana naye usiku kucha? Mwanzo 32:28.
5. Je! Danieli aliokolewa vipi kutokana na kifo alipotupwa kwenye tundu la simba? Danieli 6:10,22.
6. Je! Wale Wayahudi watatu waliokolewa au walishinda vipi tanuru ya moto? Danieli 3:16,17.
7. Je! Paulo na Sila waliokolewa vipi kutoka mikononi mikali ya Warumi? Matendo 16:25,26.

8. Je! Yeremia aliokolewa vipi kutokana na kifo alipotupwa shimoni? Yeremia 38:6-13.
9. Je! Kama sisi, wana wa Elohim, tutakuwa waaminifu hadi mwisho na tushinde, tutapata nini? Yakobo 1:12; 1 Petro 5:4.
10. Je! Masihi aliwaahidia nini washindi? Ufunuo 2:7,11,17,26.
11. Je! Wenye haki waliokolewa vipi wakati wa utawala wa nguvu ya Upapa? Ufunuo 12:11.

**Maelezo.** Manabii walishinda na wakaokolewa kupitia maombi na uaminifu wao. Yakobo alikuwa mshindi alipopambana na malaika. Hakumshinda malaika zaidi kama vile watakatifu walishinda Upapa, lakini hawakukubali kujisalimisha, na hivyo wakawa washindi. Baba wa Mbinguni anawatuma malaika wake kutoka mbinguni ili kutupa nguvu na uwezo wa kushinda, tunapomtegemea Yeye, badala ya kutegemea nguzu za kibinadamu.

*******************************

**Somo la Januari 10, 2026 (Tevet 21, 5786).**

## CHANZO NA UMUHUMI WA UNABII WA BIBILIA

**Somo Kuu: 2 Petro 1: 1-21.**
**Fungu La Kukariri: 2 Petro 1:21.**

1. Je! Maandiko yote yamepeanwa aje? 2 Timotheo 3:16.
2. Je! Yamepeanwa kwa kusudi gani? 2 Timotheo 3:17.
3. Je! Unabii huu ni wetu wakati wa leo? Na hutafanya nini? Kumbukumbu la Torati 29:29.
4. Je! Kitabu cha mwisho katika Bibilia kinaitwa aje? Ufunuo 1: 1.
5. Je! Bwana Elohim aliwaahidi nini wale wanaosoma unabii huu? Ufunuo 1: 3.
6. Unabii wa Agano la Kale humepeanwa aje? 2 Petro 1:21.
7. Je! Ni nini imesemekana kuhusu tafsiri ya huu unabii? 2 Petro 1:20.
8. Je! Roho wa Masihi alikuwa na uhusiano wowote na manabii? 1 Petro 1:11.
9. Kuja kwa Masihi kulifunuliwaje kwake Petro? 1 Petro 1:11, 12.
10. Je! Unabii huu ni nini kwetu katika siku za leo? 2 Petro 1:19; 1 Wakorintho 10:11; Warumi 15: 4.
11. Je! Mtu wa kweli aliyechaguliwa, aliyeitwa na Baba wa Mbingu kwa uzima wa milele, atakuwa mwenye mazao au asiyezaa matunda katika kazi ya Bwana wakati huu? 2 Petro 1: 8.

******************************

**Somo la Januari 17, 2026 (Tevet 28, 5786).**

# MBIO YA USHINDI

**Somo Kuu: Zaburi 19**
**Fungu La Kukariri: Isaya 40:31**

1. Jinsi gani tumeshauriwa kukimbia mbio hii? Waebr 12: 1, sehemu ya mwisho.
2. Katika kukimbia, ni vitu gani viwili tunapaswa kuweka kando? Mstari1 sehemu ya kati.
3. Jinsi gani idadi ya mashahidi wetu imeelezewa? Mstari wa 1, sehemu ya kwanza.
4. Tunapaswa kumtazama nani tunapokimbia katika mbio hii? Mstari wa 2, sehemu ya kwanza.

5. Je! Mtazamo wa Sulemani na Paulo kuhusu wale wanaokimbia katika mbio hii ulikuwa nini? Mhu. 9:11, sehemu ya kwanza, Warumi 9:16
6. Jinsi gani utukufu wa Elohim, kama ulivyofunuliwa katika sayari za mbinguni, umeelezewa? Zab. 19: 1-3
7. Je! Utukufu huu umeenea kwa kiwango gani? Mistari 4,6
8. Je! Kwenda kwao kunalinganishwaje na yule anayekimbia katika mbio? Mistari 5.

   **Maelezo**: - Mashindano haya sio kwa mwenye mbio, wala vita sio vya wenye nguvu. Walakini Mfalme Daudi anaonyesha kwamba inahitajika mtu mwenye nguvu kukimbia mbio. Mhu. 9:11 inawakilisha wale wanaofanya juhudi kiasi mwanzoni mwa mbio zao bali kwa haraka wanaangukia majaribuni, wakati Warumi 9:16 inawakilisha wale wanaotambua udhaifu wao na wanatafuta nguvu kila siku katika madhabahu ya maombi hili kuvumilia.

9. Ni swali gani muhimu ambalo Paulo aliwauliza Wakorintho kuhusu mbio? 1 WaKor. 9:24. Sehemu ya kwanza.
10. Walishauriwa kukimbia aje? aya ya 24, sehemu ya mwisho.

    **Maelezo**. Hakutakuwa na namba 2, 3 au zawadi za faraja mwishoni mwa mbio hii. Wote watakaopokea uzima wa milele lazima wawe washindi.

11. Je! Ni nini kinachohitajika kwa wale ambao wangeshinda katika mbio hii? Mstari wa 25
12. Je! Paulo alikimbia na kupigana ili kushinda katika mbio hii? aya ya 26
13. Je! Ni nini kilichosemwa kwa wale wanaomsubiri Bwana? Isaya 40:31

******************************

**Somo la Januari 24, 2026 (Shevat 6, 5786).**

## KUKUA KATIKA NEEMA

**Somo Kuu: Waefeso 4**
**Fungu La Kukariri: Wagalatia 2:20.**

1. Je! Lengo letu kuu kama WaMasihi ni lipi? 2 Yohana 3:2, 3.
2. Ili kumwona Elohim ni nini tunafaa kuwa nayo? Waebrania 12:14.
3. Katika kuvaa utu upya jinsi gani tutakuwa? Waefeso 4:24.
4. Ushuhuda wetu kwa ulimwengu ni upi? Wagalatia 2:20.
5. Ni kupitia hatua zipi tutaweza kukua? 2 Petro 1:5-7.
6. Jinsi gani imani ni muhimu kwa MMasihi? Waebrania 11:6.
7. Je, mwito wetu mkuu ni upi? 2 Petro 1:3; Wafilipi 3:14.
8. Tukiisha kupata imani na wema, ni nini tunafaa kutafuta kwa bidii? 2 Petro 1:5; Wakolosai 2:2, 3.
9. Maarifa yatatuongoza kwa nani? 2 Petro 1:6; 1Wakorintho 9:24-27.
10. Ni nini itafuatia ikiwa tutafikia kiwango cha uMasihi? Yohana 17:21-23.
11. Ni nini kitakachotokea kutokana na kukua katika neema? 2 Petro 1:8.
12. Ikiwa tutashindwa katika mambo haya, ni nini tutakuwa tumesahau? 2 Petro 1:9.

******************************

**Somo la Januari 31, 2026 (Shevat 13, 5786).**
**ADUI**

**Somo Kuu: Ufunuo 20**
**Fungu La Kukariri: Yakobo 4:7**

1. Je, ni majina yapi yamepewa adui wetu? Ufunuo 12:9.
2. Ni katika hali gani adui wa nafsi zetu ametajwa kwanza? Mwanzo 3:1-6.
3. Je! Ni wapi Yahshua aliona Shetani akianguka kutoka? Luka 10:18.
4. Ni nani ambaye alifukuzwa kutoka mbinguni pamoja na Shetani? Ufunuo 12:7-9.
5. Je, Elohim aliwasemehe malaika ambao walitenda dhambi? 2 Petro 2:4; Yuda, mstari wa 6.
6. Je! Baba ya uongo na pia muuaji wa kwanza ni nani? Yohana 8:44.
7. Ni katika tabia gani adui yetu kwa wakati mwingine huja? 1 Petro 5:8.
8. Ni katika njia gani ya uongo yeye anaonekana katika nyakati zingine? 2 Wakorintho 11:14, 15.
9. Je, inawezekana kwa ibilisi kuwatega watu? 2 Timotheo 2:26.
10. Je, Mwana wa Elohim alikuwa huru kutokana na majaribu? Luka 4:1-3; Waebrania 4:15.
11. Ni nani mwanzilishi wa dhambi? 1 Yohana 3:8.
12. Ni nani mshitaki wa ndugu zetu? Ufunuo 12:10.
13. Ni wapi ambapo Shetani atakuwa wakati wa miaka elfu moja, wakati Masihi atakuwa akitawala katika kiti cha enzi cha Daudi? Ufunuo 20:1-3.
14. Ni nini imesemwa kuhusu adhabu ya mwisho ya Shetani? Ufunuo 20:10.
15. Ni kwa ajili ya nani ziwa la moto limewekwa tayari? Mathayo 25: 4.

******************************

**Somo la Februari 7, 2026 (Shevat 20, 5786).**
## TINI NZURI NA TINI MBAYA

**Somo Kuu: Yeremia 24.**
**Fungu La Kukariri: Yeremia 24: 7.**

1. Tini nzuri ni aina gani? Yer. 24: 5-6.
2. Je, tini nzuri zilifaa kupokelewa bora zaidi kuliko zile zilizo mbaya? Mstari wa 7.
3. Je! Ni sehemu gani ya Yuda iliwakilishwa na tini mbaya? Mstari wa 8.
4. Je, jinsi gani tini mbaya zilifaa kuadhibiwa, na je, kuna yoyote ingebaki? Mstari wa 9 na 10.

   **Maelezo**: Kutoka kwa maandiko yaliyotangulia ni wazi kwamba kulikuwa na makundi mawili tofauti ya Wayahudi katika uhamisho, na ahadi zilikuwa tofauti kwa kila kundi. Yeye bado anaweza kutenganisha nzuri kutoka kwa mbaya, kama ilivyofanyika wakati wa kale, Yeye anafanya hivyo leo.

5. Ni kundi gani la Wayahudi lilipaswa kuchaguliwa ili kujenga miji iliyokuwa ukiwa na kufanya kazi ambayo tunaona inaendelea hapa sasa? Yeremia 24: 1-7.
6. Ni mapigo mangapi yalifanyika katika kuharibu ufalme wa Yuda? Ezekieli 21: 25-27. Linganisha 2 Mambo ya Nyakati 36: 15-19.

**Maelezo**: Huwa inasemekana juu ya maadui wa mataifa kwa Israeli: "Kama ulivyotenda ndivyo utakavyotendewa." - Obadia 1:15; Yoeli anasema: "Nitakurudishia malipo yenu juu ya kichwa chako mwenyewe." - Yoeli 3: 7.

7. Katika uharibifu huu wa ufalme wa Israeli miaka 2,500 iliyopita, wale waliolinganishwa na tini mbaya walichukuliwa kwanza au mwisho? Linganisha Yer. 24: 8 na 2 Mambo ya Nyakati 36: 11, 12, 16.

   **Maelezo**: Zedekia na wakuu wake walikuwa ni tini mbaya, na waliachwa, wakati tini nzuri ziliondolewa, kama itakapokuwa mwishoni, mema yatachukuliwa kwanza.
8. Ni lini tini nzuri, ikiwa ni pamoja na Danieli na wenzake, na wengine wengi walichukuliwa? Danieli 1: 1-6.

   **Maelezo**: Waliondolewa na Mfalme Yehoyakimu na hawakuachwa Yerusalemu wakati uharibifu mbaya ulikuja ambapo wanaume, wanawake na watoto walitolewa kwa upanga.
9. Ni nini hasa kinachosemwa kuhusu tabia ya mlo wa Danieli? Danieli 1: 7-8.
10. Kabla ya uharibifu mkubwa wa waovu mwishoni mwa kipindi cha mataifa, je, watakatifu watakusanywa kwanza? Ufunuo 14:18.
11. Baada ya mkusanyiko wa matunda umekusanyika basi ni nini kitachotokea kwa waovu ikilinganishwa na mzabibu wa dunia? Mstari wa 19 na 20.
12. Ni wapi tunaambiwa kuwa watakatifu watakuwa, ambao wana ushindi juu ya mnyama na sanamu yake, wakati mapigo yatamwagwa? Ufunuo 15:1-6.

    **Maelezo**: Angalia hasa mstari wa 5 inasema: "Baada ya hayo", yaani, baada ya watakatifu walipoonekana mahali hapa ambapo ilionekana kama bahari ya kioo kwa nabii, aliwaona malaika wakitoka na mapigo saba ya mwisho - Mstari wa 6. Baini pia vita ya Armageddon vinakuja katika wakati wa pigo la sita. - Ufunuo 16: 12-15. Kwa hivyo wenye haki wanaonekana wamekusanyika mahali fulani katika ukombozi kutoka kwa maafa haya. Hakuna kitu ambacho kimesemwa mahali hapa ni wapi, wala haimaanishi kuwa walichukuliwa juu kama tunavyosikia mara nyingi ikinukuliwa.

*****************************

**Somo la Februari 14, 2026 (Shevat 27, 5786).**

## KAMA ILIVYOKUWA SIKU ZA NUHU

**Somo Kuu: Mathayo 24:1-51.**
**Fungu la kukariri: Mathayo 24:37.**

1. Wakati mmoja Yahshua alikuwa katika mlima wa mizeituni, wanafunzi wake walimuuliza kuhusu nini? Mathayo. 24:3.
2. Jinsi gani Yahshua alifananisha siku kabla ya kurudi kwake? Mathayo 24:37.
3. Baadhi ya dhambi wakati wa siku za Nuhu zilikuwa gani? Mathayo. 24:38; Luke 17:26-27.
4. Ni uovu gani wa binadamu unaoelezewa katika kitabu cha mwanzo 6:2, 5, 11-13?
5. Katika maovu katika hizo siku, ni nani pekee yake, na nyumba yake walibaki kuwa waaminifu? Mwanzo. 7:1.
6. Mtume Paulo alizungumza nini kuhusu Nuhu? Waebrania. 11:7.

7. Ni kupitia kwa nani Elohim alionya watu katika wakati huo, wakati maasi yalikuwa makubwa? 2 Petro. 2:5.
8. Nini kilitokea baada ya Bwana kumwita Nuhu na watu wa nyumba yake katika safina? Mwanzo. 7:4, 11-12.
9. Ni kwa kiwango gani kulikuwa na ukamilifu katika kuangamiza viumbe viote? Mwanzo. 7:21-23.
10. Ni kwa nani Petro alizungumza kuwa uharibifu wa wakati wa Nuhu na Lutu, umetolewa kama mfano? 2 Petro 2:5, 6.
11. Dunia ovu iliangamizwa kwa maji wakati wa Nuhu. Maandiko yanasemaje, ni nini kitatokea kwa Dunia ovu wakati ujao? 2 Petro 3:6,7,10.
12. Baada ya dhambi na watenda dhambi kuwa wameharibiwa, na dunia kuwa imesafishwa kwa moto, nini kitakuwa kimekamilika? 2 Petro3:11-13; Isaya. 65:17.

*******************************

**Somo la Februari 21, 2026 (Adar 4, 5786).**

## HALI YA SIKU ZA MWISHO KUTABIRIWA

**Somo Kuu: 2 Tim. Sura ya 3.**
**Fungu La Kukariri: 2 Tim.3:14.**

1. Elezea kuhusu nyakati za hatari ambazo Paulo alinena na ni lini zitatukia? 2 Tim.3: 1-7.
2. Paulo alimaanisha nini katika aya ya 7?
3. Je! Kuna wakati unakuja ambapo kutakuwa na watu wachache ambao ni wadanganyaji? Mstari wa 13.
4. Ni kwa manufaa gani Paulo alisema kwamba maandiko haya yaliandikwa? Mstari wa 16-17.
5. Je! Watu wengine wanaofikiria kuwa ni wana wa Elohim watakuwa wakifanya nini siku za mwisho? 1 Tim.4: 1.
6. Watakuwa wakisema nini, na ni kwa nini? 1 Tim.4: 2.
7. Je! Ni nini itakuwa hali ya watu matajiri katika siku za mwisho? Yakobo 5: 1-3.
8. Kando na kuishi katika anasa, wao walifanya nini? Mstari wa 6.
9. Je! Yakobo aliwaambia ndugu ambao ni waaminifu wafanye nini? Mstari wa 7-13.
10. Katika nyakati hizi za hatari, Yahshua alisema ni nini tunapaswa kuangalia? Luka 21:34, 35.
11. Je, ni maagizo gani Paulo alitoa kwa Kanisa katika siku hizi za mwisho? Waebr.10:25.
12. Je! Watu wa dunia watafanyaje wakati Mwana wa Adamu atakapofunuliwa akishuka kutoka Mbinguni pamoja na malaika wote wenye nguvu pamoja naye? Ufunuo 6: 12-17; Mat. 24:30.

**Maelezo**: Ni wazi kutokana na ishara zote zinazotuhusu kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Nyakati za hatari ziko hapa, na ni lazima tuinue vichwa vyetu kwa sababu ukombozi wetu unakaribia. Luka 21:28. Pia kufanya kazi ya Baba yetu, kama watumishi wenye faida kwa Bwana. Mat: 24: 19-30.

*****************************

**Somo la Februari 28, 2026 (Adar 11, 5786).**
**ISHARA ZA KUJA KWAKE**

**Somo Kuu: Luka 21: 24-36.**
**Fungu La Kukariri: Luka 21:36.**

1. Je! Inawezekana kwa mtu kujua wakati halisi wa kuja kwa pili kwa Masihi? Mathayo 24:36.
2. Je! Watu wa dunia watapata onyo lolote la tukio hili kuu? Luka 21:25.
3. Je, ni nini itakuwa hali ya ulimwengu kabla ya kurudi kwa Bwana? Luka 21:25, 26.
4. Wakati ishara hizi zitaanza kutokea ni nini itaonekana na watu, na wana wa Elohim watafanyaje? Luka 21:27, 28.
5. Je, ni nini kilichosemwa kuhusu hali ya Yerusalemu wakati injili itakapokuwa ikienda kwa mataifa yote? Mstari wa 24.
6. Je! Ni nini itadhihirisha wakati Yerusalemu itakoma kukanyangwa na mataifa? Mstari wa 24.
7. Je, Ni nini hali nyingine leo (kando na Wayahudi kurudi katika nchi ya Ahadi) itatuonyesha kwamba mwisho hu karibu sana? Mstari wa 25.
8. Mtume Yohana alisemaje kuwa hali ya ulimwengu kabla ya mwisho? Ufunuo 11:18.
9. Ni ishara gani ambazo zinapaswa kuangaliwa katika nguvu za asili? Mathayo 24: 7.

   **Maelezo**. - Katika Amerika peke yake uhalifu mkubwa hutendeka kila sekunde ishirini. Hakujawahi kuonekana nyakati kama hizi za hatari. Wanasayansi sasa wanaogopa na wanatabiri uharibifu kwa vita vya atomiki.
10. Je, ni hali gani itakuwa katika dini na jamii kabla ya kurudi kwake? 2 Timotheo 3: 1-5.
11. Je, malaika alimwambia Danieli nini kuhusu nyakati zetu zenye ujuzi wa kiwango cha juu? Danieli 12: 4.

******************************

**Somo la Machi 7, 2026 (Adar 18, 5786).**
**UFALME WA ELOHIM U KARIBU, NDIO HATA MLANGONI**

**Somo Kuu: Luka 21: 24-36.**
**Fungu La Kukariri: Luka 21:36.**

1. Wayahudi walikuwa wakae kwa muda gani katika sehemu zote za ulimwengu katika kutawanyishwa kwao, na Yerusalemu kukanyangwa na watu wa mataifa? Luka 21:24.
2. Injili ya ufalme ilikuwa na uhusiano gani, hadi mwisho wa wakati? Mathayo. 24:14.
3. Wakati Wayahudi walipotawanyishwa katika mataifa yote, watu wa mataifa walikuwa wabarikiwe kwa habari njema ya ufalme huu ujao? Mathayo. 24:14.
4. Kama injili hii inakaribia kufika mwisho kwa watu wa mataifa, na Wayahudi watakapokuwa wamerejeshwa tena katika nchi yao, ni hali gani tunayoambiwa itakuwapo duniani? Luka 21:25.
5. Je, ni nini kinachosemwa kuhusu watu kuogopa mambo ambayo yatakuja kutokea? Mstari wa 26.
6. Ni hali gani za mwisho zilizotajwa, kuhusiana na mbingu kabla ya Bwana Yahshua kuonekana kuja katika mawingu? Sehemu ya mwisho ya mistari 26, 27.

**Maelezo**. Mioyo ya watu sasa imejawa na hofu, ya kuangamizwa kwa mabomu ya atomiki na hidrojeni. Nishati inakuwa tatizo kubwa sana, na matukio mengine mengi yenye kutisha yanayotokea, ambayo yote huongeza mkanganyiko ambao utakuwapo katika siku za mwisho.

7. Je, mabaki ya waumini watakuwa na wasiwasi na huzuni wakati mambo haya yatakuwa yakitokea duniani? V. 28.
8. Yahshua alitumia mfano gani rahisi? Mistari. 29-31.
9. Je! Kizazi cha watu watakaoona kurudi kwa Wayahudi kutoka uhamisho kati ya watu wa mataifa, na shida ya mataifa inayofuatia, wataishi kuona kurudi kwa Bwana wetu na Mwokozi Yahshua Masihi? Mstari wa 32.
10. Kuna njia yoyote ambayo tunaweza kuhesabu idadi ya miaka katika kizazi kimoja? Mathayo. 1:17.

**Maelezo**. Ilikuwa miaka 1,890 kabla ya Masihi wakati jina la Abramu lilibadilishwa kuwa Ibrahimu, na agano lililofanywa pamoja naye. Tunaambiwa kuwa kuna vizazi 42 katika kipindi hicho kizima, kwa hivyo kuna miaka 45 katika kizazi kimoja. Ni muhimu kuelewa kwamba hii ni sawa na "muda wa kusubiri" uliotolewa na Gabriel kwa Danieli (Danieli 12:12), wakati Daniel angefufuliwa. Ni ajabu kujua kwamba sisi tunakaribia wakati ambapo Bwana Yahshua atarudi.

******************************

**Somo la Machi 14, 2026 (Adar 25, 5786).**
**HAKIMU WA DUNIA YOTE**

**Somo Kuu: Mwanzo 18:16-33.**
**Fungu La Kukariri: Mwanzo 18:25.**

1. Katika uharibifu wa Sodoma na Gomora, ni nini imesemwa kuhusu wenye haki kuepuka hukumu? Mwanzo 18:23-32.
2. Nini imesemwa kuhusu miji hiyo kuwa mifano ya hukumu ya baadaye? 2 Petro 2:6.
3. Tunafaa kuhofu au tunafaa kuuliza swali juu ya hukumu ya Baba yetu wa Mbinguni? Zaburi 96:10; 1 Yohana 4:16-18.
4. Tunafaa kuogopa vile watu wanaweza kutufanyia, au badala yake kuchagua kuanguka katika mikono ya Baba wa mbinguni mwenye huruma? 2 Samweli 24:13, 14.

**Maelezo**: Daudi kutoka akiwa kijana, hakuishi kwa ajili yake mwenyewe. Madhumuni ya maisha yake bila hofu ya vile adui angeweza kufanya, ilikuwa ni kuwabariki wengine. Yeye alikuwa na ushahidi wa uwepo wake na mkono wenye nguvu za kuleta ukombozi. Akamwua simba na dubu, (1 Samweli 17:34-36), na akawa na nguvu juu ya jitu kubwa la Wafilisti, (mistari 48, 49), — hakuogopa kile watu wangefanya.

5. Wakati uwepo wa Baba hu pamoja nasi, mambo yataenda vizuri kila wakati? Waebrania12:6, 1 Petro 1:7.
6. Vipi kuhusu Ayubu aliyepoteza mali yake, na watoto wake wote? Ayubu 1:20-22.
7. Wakati mwili wake uliteseka sana, alipoteza imani na kulalamika? Ayubu 7:20, 21.

**Maelezo**: Ni vizuri kutambua maisha ya unyenyekevu wa Mwokozi, na tazama umaskini wake; Mateso yake katika Gethsemani; Kuaibishwa mbele ya waliomdhihaki; taji la

miiba mikali juu ya kichwa chake; Kesi na hukumu mbele ya watu waovu kama mhalifu na uchungu wake juu ya msalaba. Lakini kwa hayo yote aliibuka kuwa mshindi, na kuinuliwa mbele ya mkuu sana wa mbinguni, na kupewa taji kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.

8. Ayubu alielewa sababu ya mateso haya, au alijaribu kujifanya kuwa mwenye haki? Ayubu 31: 3-7, 24-27, na 29, 30.
9. Je! Ni nani ambaye alikuja kwa Ayubu na maneno ya faraja, na kutamka unabii ambao ulitimizwa baadaye? Ayubu 32: 5-10
10. Baadhi ya maneno hayo ya faraja yalikuwa yapi? Ayubu 33: 22-29.
11. Katika kujisalimisha na unyenyekevu wake, Ayubu hatimaye alisema nini? Ayubu 40: 3, 4; 42: 1-6. Tafadhali Soma 1 Petro 4:12, 13, na 5:6, 7.
12. Ni nini imesemwa kuhusu mtu yule ambaye huadhibiwa na Baba? Zaburi 94:2-15.
13. Ni amri gani ilitolewa kwa wale watu watatu, --- ambao wangekuwa wafariji wa Ayubu? Ayubu 42: 7-9.

    **Maelezo**: Watu hao watatu ambao walikuja kama marafiki wa Ayubu walimhukumu visivyo katika kipindi cha dhiki yake. Ghadhabu ya Elohim ikawaka juu yao. Gadhabu haikuondolewa hadi Ayubu alipoomba kwa ajili yao.
14. Baada Ayubu kuvumilia kwa subira, na kuomba kwa ajili ya marafiki zake, alibarikiwa vipi? Aya ya 10-16.
15. Ni nini imesemwa kuhusu rehema na hukumu katika Yakobo 2:12, 13?
16. Mtoto Samweli alipoachishwa maziwa, na mama yake kumpeleka mbele ya Eli kuhani. Ni maneno gani ya kinabii aliyoyazungumza kuhusu hakimu wa dunia? 1 Samweli2:10.
17. Je, mfalme Daudi aliutaraji sana wakati huo? Zaburi 94:1-3; 96:10-13.
18. Je, hitimisho ya yote ambayo yanatarajiwa kutoka kwa wanadamu ni ipi, na je, hakimu Mkuu anajua yote yaliyo sirini? Mhubiri. 12:13, 14.

******************************

## Somo la Machi 21, 2026 (Abib 3, 5786).
## NYUMBANI MWA WALIO-OKOLEWA

**Somo Kuu: Ufunuo 21.**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 21:27.**

1. Je! Nyumba ya wakati ujao ya waliookolewa itapatikana wapi? Mathayo 5:5; Mithali 10:30; Ufunuo 5:9,10.

    **Maelezo.** Bwana Yahshua aliwaambia wanafunzi Wake waombee Ufalme uje ili mapenzi ya Baba yatimizwe duniani kama ilivyo mbinguni. (Mathayo 6:9,10). Dunia hii haikuumbwa ili ikaliwe milele na watu wenye pupa, wabinafsi, wenye kutamani mali, wanaopenda vita, na kila aina ya wenye dhambi. Muumba ana uwezo wa kuleta mabadiliko haya yanayokuja, na sasa yako karibu sana. Ingawa itahitaji uharibifu mkubwa wa maisha na mali ili kusafisha dunia ya dhambi na wenye dhambi, ni hakika itakuja na wakati huu kwa moto badala ya maji kama ilivyokuwa siku za Nuhu.
2. Ni nani atakuwa mfalme juu ya dunia yote wakati wa urejesho, au kurudisha dunia katika hali yake ya Edeni? Ufunuo 11:15; Isaya 24:23; Zaburi 110:1-6.

3. Je! Yahshua alisema nini kuhusu maandalizi ya waliookolewa, na nyumba ya Baba Yake? Yohana 14:1-3.

   **Maelezo.** Yahshua hakusema atawatuma wengine kuwachukua waliookolewa waende mahali alipokuwa anaenda. Bali alisema, "Nitakuja tena, na kuwapokea kwangu mwenyewe; ili mlipo mimi, ninyi pia muwepo." Tumeambiwa katika mahali kwingi kwamba atakaporudi, atakuwa Mfalme na atatawala duniani. Ufalme wa dunia hii utakuwa Wake. Alizaliwa kwa kusudi hili. Isaya 9:6,7.
4. Je! Ni nini kitawatokea wenye haki ili kuwapa uzima wa milele? 1 Wakorintho 15:51-53.
5. Je! Ni njia gani ya sasa ambayo uzima na afya zitapewa waliookolewa? Ufunuo 22:2.
6. Je, tutaungana tena na wapendwa wetu? Yeremia 31:16,17.
7. Je, miili yetu itabadilishwa na kuwa sawa na mwili wa kiroho wa Masihi? Wafilipi 3:20,21.

   **Maelezo.** Baada ya Yahshua kufufuliwa kutoka kwa wafu, na hivyo kumiliki mwili huu usiokufa; Alitembea na mitume Wake hadi mji wa Emau maili nane kaskazini-magharibi mwa Yerusalemu. Pia alikula pamoja nao, lakini macho yao yalizuiliwa ili wasimtambue alipokuwa njiani. Kwa hivyo, alionekana sawa na hapo awali, na ilikuwa ni lazima macho ya marafiki Zake yabadilishwe, kwa sababu alionekana kama hapo awali. Kisha baadaye walimtambua. (Luka 24:28-31). Miili yetu itakapobadilishwa na kuwa kama mwili Wake mtukufu, sisi pia tutaonekana sawa na tunavyoonekana sasa, na tutawatambua wapendwa wetu, na wao watatutambua.

*******************************

**Somo la Machi 28, 2026 (Abib 10, 5786).**
**WITO WA WATUMISHI NA USAMBAZAJI WA KARAMA**

**Somo Kuu: Mathayo 25: 14-46.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 25: 19.**

1. Je! Ufalme wa Mbinguni unalinganishwa na nini, ni nani ambaye alitembea kwenda nchi ya mbali? Mathayo 25: 14.

   **Maelezo:** Masihi bado anaita watumishi kufanya kazi yake.
2. Ni nini imesemwa kuhusu usambazaji wa talanta, au karama kwa ajili ya kuongeza kundi, na kuzivuta nafsi za watu? Mathayo 25: 15.
3. Je! Mtumishi ambaye alipokea idadi kubwa ya talanta alifanya nini? Mathayo 25: 16, 17.
4. Je! Mtumishi ambaye aliyeipokea talanta moja alifanya nini? Mathayo 25: 18.
5. Nini kinachotokea baada ya muda mrefu? Mathayo 25: 19.
6. Je, wale ambao hutumia sahihi talanta walizopokea, na kuziongeza kwa ajili ya kuzivuta nafsi watapewa tuzo gani? Mathayo 25:20-23.
7. Je, ni hukumu gani aliyopewa mtumishi ambaye alificha talanta yake katika ardhi, kutokuwa na ongezeko lolote katika maisha yake kwa ajili ya utukufu wa Elohim? Mathayo 25: 24-28.
8. Badala ya kuingia katika ufalme, ni nini itasemwa kwa mtumishi asiye na faida ambaye huficha maisha yake yote katika dunia hii ya kale? Mathayo 25: 29-30.

**Maelezo**: Hivi ndivyo mamilioni wanafanya leo, kuishi kwa ajili yao wenyewe, na kuzikwa ndani kabisa katika mambo ya dunia. Wanatafuta pesa, mali, na raha, kuabudu dola tu na kile ambacho dola hutoa kwao. Mwisraeli wa kweli si hivyo. Yeye anafaa kukuza talanta yake na kuishi maisha yake kwa ajili ya ongezeko la ufalme, kutoa zaka na sadaka, na pia kuishi katika utiifu wa upendo, na kujitenga mwenyewe na ulimwengu.

9. Katika kufuata hatua za Mwokozi wetu, ni mambo ya nani yatakayotuhusu sisi zaidi? Luka 2:49.
10. Kuna kitu cha thamani zaidi kuliko chakula kwa ajili ya mwili na mavazi, ni nini itabaki kwanza kabisa katika kila nyoyo? Luka 12:23-32.
11. Ni nini kitatokea kwa maisha ya kiroho ya mtu asiye na faida ambaye huficha talanta yake, na kushindwa kutoa mazao? Luka 13:6-9.
12. Ni nini itatokea kwa mtu ambaye huweka katika akiba kwa ajili yake mwenyewe, na kuzika talanta yake katika ardhi, na si tajiri kwake Elohim? Luka 12:16-21.

******************************